

**MAJIBU YENYE FAIDA KUHUSU MIFUMO MIPYA**

## **“MAJIBU YENYE FAIDA”**

**NO.6**

**KUHUSU**

**MASWALI YANAYO FUNGAMANA NA MIFUMO MIPYA**

**MTUNZI, SHEIKH SWALEH BIN FAWZA AL FAWZAN**

**-ALLAH AMUHIFADHI-**

**MFASIRI, ABUL ‘AALIYAH UMAR BIN MUHAMMA KONDO**

**-ALLAH AMSAMEHE YEYE NA WAISLAMU WOTE -**

**PONGWE - TANGA - TANZANIA**

---

## MAJIBU YENYE FAIDA KUHUSU MIFUMO MIPYA

**Swali la sita:** Je..! anayejinasibisha kwenye haya makundi atazingatiwa ni mzushi (mtu wa bid'ah)?

**Jawabu:** Hili linategemea na makundi, (atakaejinasibisha na) makundi ambayo yana mambo yanayokwenda kinyume na kitabu (Qur'an) na sunna atazingatiwa mwenye kujinasibisha nayo ni mzushi.

**Swali la saba:** Mnaonaje kuhusu makundi kama (kupewa) hukumu yenyе kuenea?

**Jawabu:** Kila yule ambaye amekwenda kinyume na kundi la Ahlus-sunnah basi huyo ni mpotevu, hatuna sisi isipokuwa kundi ni moja tu nalo ni Ahlus-sunnah waljama'ah, na ataka elikhali fu kundi hili basi huyo (atakuwa ) ni mwenye kwenda kinyume

## MAJIBU YENYE FAIDA KUHUSU MIFUMO MIPYA

na Manhaj (njia) ya Mtume swala na salamu zimshukie.

Na tunasema tena: Kila atakaekwenda kinyume na Ahlus-sunnah waljama'ah basi huyo ni katika watu (wenye kufuata matamanio) wa matamanio,na mikhalaifa (mambo yaliyokuwa kiyume na sheria) inatofautiana katika kupewa hukumu ya kumtia mtu katika upotevu,kumtia mtu katika ukafiri,kulingana na udogo wake na ukubwa wake (upotevu huo),umbali wake na ukaribu wake na haki.